# TANZANIA TELECOMMUNICATIONS CORPORATION

## MKATABA WA KUTOA HUDUMA YA MTANDAO KWA NJIA YA FAIBA KWENYE NYUMBA ZA MAKAZI

Mkataba huu ni kati ya Shirika la Mawasiliano Tanzania, shirika la umma lililianzishwa na sheria za Tanzania iliyo na ofisi iliyosajiliwa gorofa ya 12, jengo la Extelecoms, 32 mtaa wa Samora. S.L.P 9070 Dar Es Salaam. Baada ya hapa atatambulika kama "Mtoa huduma"

Na
Mkazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya hapa atajulikana kama "mteja" .

Sasa mkataba huu unashuhudia yafuatayo:

1. Mtoa huduma anakubali kutoa huduma ya intaneti kwa kutumia teknolojia ya faiba kwa mteja na mteja amekubali kununua huduma hii kwa malipo ya kabla ya kila mwezi.

2. Kasi ya intaneti ya kutumia pamoja itakuwa na kasi kwa sekunde na muda wowote ule mteja ataweza kuomba kupunguziwa kifurushi chake au kuongeza isipokuwa pale ambapo mteja amenunua kifurushi cha chini kabisa.

3. Mtoa huduma ataunganisha huduma ya intaneti kwa mteja bila gharama zozote kwa mteja kwa sharti kwamba mteja atanunua intaneti kila mwezi kwa kutumia mfumo wa malipo ya serikali ambapo atatumiwa namba ya malipo kwenye namba yake ya simu ya mkononi au mfumo mwingine ambao utakuwa umekubalika awali.

4. Endapo mteja atashindwa kuomba namba ya malipo ya serikali na kutolipia huduma kwa muda wa siku 90 mfululizo, Mtoa huduma atatafsiri kwamba mkataba wa kutoa huduma hii umefikia ukomo kwa sababu mteja ameshindwa kutekeleza matakwa ya mkataba. Mtoa huduma atakuwa na uhuru wa kuchukua vifaa vilivyofungwa kwa mteja ikiwa ni pamoja na nguzo, waya na "rauta" iliyosimikwa kwenye nyumba ya mteja bila kutoa tararifa ya awali kwa Mteja.

5. Vifaa vilivyofungwa kwa mteja, kwa muda wote wa mkataba huu vitabaki kuwa ni mali ya mtoa huduma. Kwa wakati wowote mteja hatokuwa ni miliki vifaa hivyo. Mteja hatoruhusiwa kuuza, kutumia vifaa hivyo kama dhamana ya mkopo, kukodisha au kuruhusu watu ambao sio wakazi kwenye nyumba ya mteja kufahamu nenosiri.

6. Endapo mteja atahama kutoka kwenye makazi yake ya sasa kwenda kwenye makazi mengine, mteja atawajibika kutoa taarifa ya siku 30 kabla ya siku yake ya kuhama kwa Mtoa huduma. Mtoa huduma atakuwa na maamuzi ya kuhamisha vifaa kweny makazi mapya ya mteja au kukabidhi kifaa kwa mkazi mwingine atakayehamia kwenye nyumba hiyo. Hata hivyo mtoa huduma hatoi ahadi ya moja kwa moja ya kumuunganishia mteja huduma kwenye makazi yake mapya.

7. Baada ya mteja kuunganishiwa huduma, mteja atawaruhusu wafanyakazi wa mtoa huduma pale ambapo mtoa huduma ataomba, kuweza kufanya matengenezo ya vifaa.

8. Huduma inayotolewa kwa mteja ni kwa ajili ya matumizi binafsi. Mteja haruhusiwi kuuza huduma ya intaneti kwa mtu mwingine yeyote kwa namna yoyote ile ikiwa ni pamoja na kutoa nenosiri la WI-FI kwa mtu mwingine au kushirikiana kulipa ankara za mwezi. Kwa utashi wa Mtoa huduma, endapo ataona kuwa mteja anauza huduma za intaneti , mtoa huduma atakuwa na nguvu ya kuchukua vifaa kutoka kwenye makazi ya mteja kwani kitendo hicho cha kuuza huduma kitatafsiriwa kama kimevunja masharti ya mkataba huu na hatua stahiki za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mteja.

9. Vifaa vitafungwa kwenye makazi ya mteja kwenye eneo ambalo si rahisi watoto kufikia na ni salama kwa matumizi.

10. Ni rauta moja tu itafungwa kwenye makazi ya mteja. Endapo mteja atahitaji zaidi ya router moja, mteja atakuwa na jukumu ya kukodi mkandarasi ambaye atamtengenezea mtandao wa mawasiliano wa ndani ili kuwezesha router aliyofungiwa kuunganishwa kwenye vifaa vingine vya kusambazia mtandao.

11. Mteja amekubali kutumia huduma za faiba mlangoni kwa kuzingatia Sheria za Tanzania, kanuni hivyo endapo matumizi sahihi ya huduma hayatafanywa na mteja itapelekea kuvunjika kwa mkataba.

12. Mteja atakuwa na wajibu wa kutunza rauta na vifaa vingine kwa umakini mkubwa, kuchukua tahadhari wakati wote kuondoa uwezekano wa kuharibu, kupotea au kuibwa. Endapo itagundulika kuwa kifaa kimeharibika kutokana na matumizi mabaya kutoka kwa mteja, mteja atawajibika kulipia kifaa kilichoharibika.

13. Matengenezo yote yatafanywa na mtoa huduma, mteja hatoruhusiwa kufanya mabadiliko au matengenezo yoyote kwenye vifaa vilivyofungwa kwake au kukitumia kwa matumizi mengine zaidi yaliyokubalika kwenye mkataba.

14. Endapo kifaa hakifanyi kazi kama inavyotarajiwa, mteja atatoa taarifa kwenye ofisi za Mtoa huduma zilizo karibu. Marekebisho wa vifaa yatafanywa kwa garama za mtoa huduma isipokuwa pale itakapoamuliwa vinginevyo na mtoa huduma.

15. Mtoa huduma ataondoa huduma za faiba mlangoni endapo mteja atahitaji huduma hiyo iondolewe, endapo itakuwa ni hitajio la kisheria au mamlaka, au tatizo la kiufundi au masuala ya usalama, kuboresha huduma au ni uamuzi wa Mtoa huduma kusitisha huduma na hili litafanywa baada ya taarifa ya awali kutolewa kwa mteja.

16. Mtu yoyote ambaye ni sehemu ya mkataba huu hatakuwa na wajibu wowote wa kisheria endapo atashindwa kutekeleza wajibu wake kwenye mkataba huu, kama jambo lililosababisha kushindikana kutelelezwa mwa jambo hilo liko nje wa uwezo wa mtu huyo kulitenda au ni jambo la asili, endapo aliutaarifu upande mwingine wa mkataba kuwa jambo hilo halitoweza kufanyika kwa kuwa jambo ambalo liko nje ya uwezo wake limetokea.

17. Kwa ajili ya kifungu hiki mambo ambayo yako nje ya uwezo na hayasababishwi na mtu kwenye mkataba huu (force majeure) bila kubanwa na mambo yaliyoelezwa hapa kama milipuko, vita, uvamizi, tetemeko la ardhi, radi, wizi wa miundombinu ya

mtandao, vitendo vya serikali au serikali kuu, sheria za Jeshi au jambo lolote ambalo liko nje ya utawala wa mtu ambaye ameathirika nayo.

18. Mkataba huu utasimamiwa na sheria za Tanzania.
19. Kwa ajili ya kutoa taarifa, tafadhali pia kituo cha huduma kwa wateja namba **100 au 0222 100 100** au tembelea kituo kilichokaribu nawe kwa ajili ya msaada.

Ninakubali kuwa nimesoma na kuelewa masharti ya mkataba huu na ninakubaliana na masharti haya. Ninakubali kutumia huduma ya faiba mlangoni na kukubali majukumu yote kama mteja. Ninaelewa na kukubali kwamba kushindwa kutekeleza masharti ya mkataba huu kunaweza kupelekea mtoa huduma kusitisha huduma.